

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**  
**12 Julai 2008**

**Mahudhurio**

Ally Athuman Jumbe  
Ally Saidi Mohamedi  
Ally Saidi Mwishehe  
Aseli Wilison  
Dominata Rwechungura  
Edgar R Paulo  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Frank Peter Rwechungura  
Juma Ali Salehe Jongo  
Juma Ayouba Ally  
Kibwana Mohammad Msiga  
Paulo Atibu Hatibu  
Ramadhani Rajabu Nyengo

**Mradi wa Usalama Barabarani - Wamba Memorial Fund**

Filbert na Dominata walipitia jarida na wamefanya marekebisho, na Elaine atazichapa. Elaine aliweka picha ndani ya jarida. Tutaprint na tutatoa photocopy kwa ajili ya washiriki.

Elaine na Juma hawakuenda kumwona Bwana Wemba wa Chuo cha Usafirishaji wiki hii – wataenda jumatatu.

Shule ya Mbondole watapeleka watu wawili kwenye kozi – mwalimu mmoja wa shule wa msingi (Hatibu Hamisi) na mwalimu mmoja wa shule ya sekondari (Abdallah Kilonda). Ally Saidi Mohammad alisema atajua guest inaitwa Mango ambayo ni self contained na bei yake ni Tsh 5,000 kwa siku, ambapo wanaweza kukaa. Kigamboni Secondary School bado hawajajibu – Elaine atafuatalia. Juma hakuwenda HUWATA lakini atafanya wiki hii. Mpaka sasa wanachama 14 wa UWABA wamejiandikisha kuhudhuria kozi.

Andrew alijibu email kusema atapenda kutana na watu wa serekali. Juma alipeleka barua kwa TANROADS, halmashauri ya jiji na traffic police na wote walisema kwamaba anaweza kuja kutana nao alhamisi ile.

Juma na Elaine watachukua hela kutoka benki kiasi ya kutosha kwa kozi

**Ofisi**

Mejah bado hajapaka rangi kwenye ofisi mpya. Tuliamua kuhamia baada ya kozi imemaliza.

### **Mambo ya hela**

Wakati wa wiki Juma alitumia Tsh 400 kwa nauli za ferry, Tsh 1,000 kwa furueli kwa baisikeli yake anayetumia kwa kazi ya UWABA, na Tsh 50 kwa photocopying. Elaine alitumia Tsh 1,500 kuprint barua. Anabaki na Tsh 65,950 ya hela ya UWABA.